# SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 31 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) SEPTEMBA 2023

# WAZIRI KAIRUKI AITAKA TSC KUFANYIA KAZI HOJA ZILIZOWASILISHWA KWENYE MAONESHO YA NANENANE




*Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki akiongea na watumishi wa OR – TAMISEMI na Taasisi zake walioshiriki kwenye Maonesho ya Nanenane Kitaifa na Kimataifa mkoani Mbeya.*

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# WALIMU TUMIENI MFUMO WA TSCMIS ILI KUTATULIWA CHANGAMOTO ZENU KWA WAKATI NA KUEPUSHA USUMBUFU WA KUTOKA KWENYE VITUO VYA KAZI KUTAFUTA HUDUMA

Tume ya Utumishi wa Walimu imepewa dhamana kwa mujibu wa Sheria kusimamia na kuendeleza Utumishi wa Walimu nchini. Katika kutekeleza wajibu huo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, TSC imekamilisha kutengeneza Mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information system (TSCMIS) toleo la 1.0.0 wenye lengo la kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu.

Kwa mujibu wa wataalamu, mfumo huo utawaondolea walimu usumbufu wa kufuata huduma kwenye Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya na Makao Makuu badala yake mwalimu atakuwa na uwezo wa kuingia kwenye Mfumo mahali popote kwa kutumia simu janja au Kishikwambi alichopatiwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwasilisha suala au lalamiko lake kuhusu utumishi wake.

Tunaipongeza Menejimenti ya TSC ikiongozwa na Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama kwa juhudi kubwa za kuboresha upatikanaji wa huduma kwa walimu. Ni vyema watumishi wa Tume kuanzia ngazi ya Makao Makuu na wilayani kuhakikisha walimu wanatatuliwa changamoto zao kwa ubora zaidi ili malengo ya kuwepo kwa mfumo huo yaweze kufikiwa.

Mfumo huu umekusudiwa kufanya mwalimu asihangaike kutoka kwenye kituo chake cha kazi kwa ajili ya kutafuta huduma, kama atakuwa na hoja zake ataingia kwenye mfumo atatoa taarifa ataweka hoja yake atatuma. Akishatuma ana uwezo wa kufuatilia na kuona hoja yake ilipofikia na pale itakapokuwa imejibiwa atapata majibu hapo hapo. Hivyo, ni muhimu kwa kila mwalimu kuhakikisha amejisajili na kutumia mfumo huu kikamilifu ili kutatuliwa changamoto zake.

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina M. Nkwama


**Wajumbe**
Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

**Mhariri Mkuu**
Gerard J. Chami

**Mhariri**
Adili J. Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas G. Ogunde

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania   tumeyautumishiwawalimutanzania

# WAZIRI KAIRUKI AITAKA TSC KUFANYIA KAZI HOJA ZILIZOWASILISHWA KWENYE MAONESHO YA NANENANE

**Na Mwandishi wetu – Mbeya.**

Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki ameitaka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuzifanyia kazi hoja zote zilizowasilishwa na wateja ambao wengi wao ni walimu wakati wa maonesho ya wakulima Nanenane ili kuendelea kuondoa changamoto za walimu nchini.

Waziri Kairuki alitoa agizo hilo alipotembelea banda la TAMISEMI na Taasisi zake tarehe 8 Agosti, 2023 katika kilele cha maonesho ya Nanenane Kitaifa na Kimataifa yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.




*Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki akisaini Kitabu cha wageni tarehe 8 Agosti, 2023 alipotembelea banda la Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi zake kwenye Maonesho ya Nanenane Kitaifa na Kimataifa mkoani Mbeya.*

"Natambua kuwa mmepokea hoja nyingi za wateja waliotembelea kwenye banda lenu na wateja wengi ni walimu. Hoja zilizotolewa siyo za walimu wa Mkoa wa Mbeya peke yake ukienda maeneo yote utakuta ni hizohizo. Nendeni mkazichambue na kuzipatia ufumbuzi ili walimu wetu waendelee kutekeleza majukumu yao kwa amani na Utulivu," amesema Waziri Kairuki.

Akisisitiza agizo hilo, Waziri Kairuki amesema miongoni mwa kero kubwa ambazo TSC inapaswa kuzifanyia kazi ni walimu kucheleweshwa kupandishwa vyeo, kupandishwa madaraja bila kuzingatia utaratibu kitu kinachosababisha kutofautiana kwa vyeo kwa walimu wa kundi rika moja, walimu wanaopanda vyeo pamoja kuidhinishiwa barua za kupanda vyeo kwa tarehe tofauti kwa sababu za kimfumo na kucheleweshwa kubadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza kielimu.

Pamoja na hayo, Waziri Kairuki amewataka watumishi wote wa OR – TAMISEMI na taasisi zake kuendelea kufanya kazi kwa bidi, ubunifu na moyo wa kujituma ili kuendelea kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kutimiza malengo yake ya kuwaletea maendeleo wananchi.

"Ninajua watumishi wa OR - TAMISEMI pamoja na Taasisi zetu mna uwezo mzuri wa kufanya kazi na mnatekeleza majukumu yenu vizuri. Kama tunavyojua Ofisi ya Rais TAMISEMI ndiyo inayohudumia wananchi moja kwa moja, na sisi watendaji ndio tunaotegemewa katika utoaji wa huduma hizo. Hivyo, kila mmoja wetu ahakikishe anatimiza wajibu wake ipasavyo ili Rais wetu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aweze kufikia malengo yake katika kuwaletea maendeleo wananchi," amesema Waziri Kairuki.



*Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (wa tatu kutoka kushoto waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa OR – TAMISEMI na Taasisi zake walioshiriki kwenye Maonesho ya Nanenane Kitaifa na Kimataifa mkoani Mbeya.*


wa Tanzania


www.tamisemi.go.tz

# NKWAMA AWATAKA WATENDAJI WA TSC MVOMERO KUTUMIA MFUMO WA TSCMIS NA KUSAMBAZA NAKALA ZA KITABU CHA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI NA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU

**Na Mwandishi wetu – Mvomero.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amewataka watendaji wa TSC Wilaya ya Mvomero kuhakikisha wanatumia kikamilifu mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) kwenye usajili wa walimu ajira mpya na kupokea malalamiko ya walimu kuhusu upandishwaji vyeo na ubadilishwaji wa kazi/vyeo.

Pia, amewaagiza watendaji hao kusambaza nakala za Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa Wakuu wa Shule za Msingi za Wilaya hiyo ili kuongeza uelewa wa taratibu mbalimali za kiutumishi kwa walimu.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisani kitabu cha wageni katika ofisi ya TSC Wilaya ya Mvomero tarehe 10 Agosti, 2023.*

Mwl. Nkwama ameyasema hayo tarehe 10 Agosti, 2023 katika ziara yake wilayani mvomero iliyolenga kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu TSC katika Wilaya hiyo.

"TSC tumedhamiria kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa walimu, kwa sasa tumeanza kutumia mfumo wa TSCMIS katika usajili wa walimu ajira mpya na kupokea malalamiko ya walimu kuhusu upandishwaji vyeo na ubadilishwaji wa kazi/vyeo. Hivyo, hakikisheni mfumo huu mnautumia kikamilifu kulingana na maelekezo mliyopewa," amesema Mwl. Nkwama.

Pamoja na hayo, Nkwama amewasisitiza watendaji hao kuhakikisha vikao vya lazima vya kisheria vinafanyika ili kutolea maamuzi masuala mbalimbali ya TSC katika Wilaya hiyo.

Nao watendaji wa TSC Mvomero walimweleza Mwl. Nkwama kuwa changamoto zinazoikabili ofisi hiyo ni upungufu wa fedha za kuendeshea vikao vya Kisheria pamoja na kukosekana kwa mtandao wa Intaneti kwa ajili ya matumizi ya kazi za ofisi.

Akitoa ufafanuzi juu ya changamoto hizo, Mwl. Nkwama alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 TSC imepata ongezeko la bajeti kwa ajili ya vikao vya kisheria, hivyo changamoto ya upungufu wa fedha za vikao tayari imetatuliwa na kuhusu ukosefu wa mtando wa intaneti, Nkwama aliwaelekeza watendaji hao kufuatilia TTCL kuhusu upatikanaji wa Mkongo wa Taifa.

Katika ziara hiyo, Nkwama alikutana na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Mhe. Judith Nguli ambapo alimshukuru kwa kuipatia TSC vyumba viwili vya ofisi.

Mwl. Paulina Nkwama alihitimisha ziara yake wilayani hapo kwa kufika na kuzungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero Mwl. Lino Mwigeni na kumshukuru kwa kuipatia TSC Wilaya ya Mvomero kiwanja cha takribani hekari mbili (2) kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Tume wilayani hapo.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye miwani) akiwa katika kikao na watendaji wa TSC Mvomero tarehe 10 Agosti, 2023.*



# KATIBU MKUU MWELI AIPONGEZA TSC KWA KUKAMILISHA MFUMO WA TSCMIS



*Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli (wa kwaza kushoto) akizungumza na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kushoto) pamoja na watumishi wengine wa TSC waliokuwa wanatoa huduma kwenye Maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya.*

**Na Mwandishi Wetu – Mbeya.**

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kukamilisha mfumo wa kielektoniki ujulikanao kama Teachers Service Commission Management Information System (TSCMIS) ambao unalenga kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu.

Katibu Mkuu Mweli ametoa pongezi hizo tarehe 7 Agosti, 2023 alipotembelea Banda la TSC katika Maonesho ya Wakulima NaneNane Kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.

Mweli amesema kwa muda mrefu walimu wamekuwa akitumia muda na gharama kwa ajili ya kufika katika ofisi za Serikali kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili, kitu ambacho siyo kwamba kinawapa walimu usumbufu tu bali kinawanyima wanafunzi haki ya kufundishwa kama inavyotakiwa.

"Ninawapongeza sana TSC kwa kukamilisha mfumo huu ambao utawasaidia sana walimu wetu. Lengo la Serikali ni kuhakikisha mwalimu anatulia darasani na kufundisha, hivyo TSCMIS inampatia mwalimu fursa ya kupata huduma zake za kiutumishi bila kutoka kwenye kituo chake cha kazi. Ninaomba mtumie mfumo huu ipasavyo kwa ajili ya kuwasaidia walimu," amesema Katibu Mkuu huyo.

Akitoa ufafanuzi kwa Katibu Mkuu huyo, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama amesema ujenzi wa Mfumo wa TSCMIS ulichukua muda wa miaka miwili hadi kukamilika ambapo ujenzi wake ulihusisha wataalam kutoka Taasisi mbalimbali ikiwewo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mamlaka ya Serikali Mtandao na Vyuo Vikuu vya Sokoine na Mzumbe.

Amesema mfumo huo una moduli sita ambazo ni Disciplinary (Mashauri ya Nidhamu), Appeal (Rufaa), Gratuity and Pension Computation (Mafao na Pession), Complaints (Malalamiko), Registration (Usajili) na Visitors and Helpdesk (Wageni na dawati la usaidizi).

"Mfumo wa TSCMIS utarahisisha na kuboresha utendaji kazi wa shughuli za kila siku katika kuwahudumia walimu kwenye masuala ya ajira (usajili na kuthibitishwa kazini), maendeleo ya Walimu (kupandishwa vyeo na kubadilishiwa muundo wa utumishi), mafao, mashauri ya nidhamu pamoja na rufaa za walimu," amesema Nkwama.




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi kuhusu mfumo wa kielektoniki ujulikanao kama Teachers Service Commission Management Information System (TSCMIS) kwa Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli wakati wa maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya.*





*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akimuonesha jambo Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli wakati wa maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya tarehe 7 Agosti, 2023.*

*Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli akiwa katika picha ya pamoja na watumishi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi zake wakati alipotembelea mabanda ya Ofisi hiyo tarehe 7 Agosti, 2023 katika maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya.*







*Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Fatuma Muya akitoa huduma kwa wateja waliotembelea banda la TSC tarehe 6 Julai, 2023 katika maonesho ya Wakulima Nanenane yaliyofanyia Kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.*




*Watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake walioshiriki maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya wakiwa aktika picha ya pamoja na wateja waliotembelea mabanda ya TAMISEMI.*





*Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakihudumia wateja waliotembelea banda la TSC kwenye Maonesho ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika Agosti 1 – 8, 2023 katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.*

# KATIBU TSC AFANYA ZIARA OFISI YA TSC WILAYA YA KILOSA

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, tarehe 11/8/2023 alitembelea Ofisi za TSC Wilaya ya Kilosa na kuzungumza na watumishi juu ya mafanikio na changamoto zinanzoikabili ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.

Taarifa ya ziara ya Kiongozi huyo imeeleza kwamba akiwa ofisini hapo, Katibu huyo alipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika Wilaya hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016 iliyowasilishwa na Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kilosa, Bw. Daudi Mchillu.

Mchillu alibainisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho kuwa ni usajili, upandishwaji vyeo, kuwabadilishia vyeo/kazi, kutoa vibali vya kustaafu, kuhuisha Tange ya kila mwaka pamoja na kushughulikia masuala ya kinidhamu.

"Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na, ukarabati wa ofisi, ongezeko la mtumishi, matumizi ya TEHAMA na ushirikiano mzuri baina ya ofisi ya TSC Kilosa na ofisi nyingine ikiwemo ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kilosa," ilieleza sehemu ya taarifa ya ziara ya Kiongozi huyo.

Mchillu alifafanua kuwa changamoto kubwa zinazoikabili ofisi hiyo ni ufinyu wa bajeti na Jiografia ya kuzifikia baadhi ya shule za wilaya hiyo.

Hata hivyo, Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kwamba Ofisi ya Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, wamekuwa wakitatua changamoto hizo kwa pamoja kwa kutumia vyombo vya usafiri pamoja na wataalamu wa Halmashauri kuzifikia shule hizo.

Aidha, Mwl. Nkwama alizungumzua utatuzi wa changamoto ya ufinyu wa bajeti ambapo alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 Tume ya Utumishi wa Walimu imeongezewa fedha kwa ajili ya vikao vya kisheria hivyo, baadhi ya changamoto za kibajeti zitatatuliwa.

Katika hatua nyingine, Mwl. Nkwama aliwasisitiza watendaji wa ofisi hiyo kuongeza kasi ya kusajili walimu kwenye mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) pamoja na usambazaji wa nakala za Kitabu cha Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa kuanza na Wakuu wa Shule za Msingi ambazo zinatekeleza Mradi wa BOOST.

Wilaya ya Kilosa ina Walimu 2,445 wanaohudumiwa na TSC wakiwemo 1,605 wa shule za msingi na 840 wa shule za sekondari.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC) Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kulia) akiwa katika kikao na Watumishi wa Elimu Mkoa wa Morogoro. Pichani, wa pili kushoto ni Afisa Elimu wa Mkoa wa Morogoro, Mwl. Germana Mung'aho, wa kwanza kushoto ni Afisa Elimu Sekondari Manispaa ya Morogoro na wa pili upande wa kulia ni Afisa taaluma wa Mkoa huo.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kilosa.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC) Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya ya Kilosa kutoka kwa Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kilosa, Bw. Daudi Mchillu.*



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akiagana na Katibu Tawala Msaidizi Anayeshughulikia Elimu Mkoa wa Morogoro, Mwl. Germana Mung'aho baada ya kufika Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro akiwa katika ziara ya kuzitembelea ofisi za TSC Wilaya ya Gairo, Mvomero na Kilosa.*



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akiagana na Kaimu Katibu Msaidizi na watumishi wa TSC Wilaya ya Kilosa mara baada ya kuhitimisha ziara yake katika ofisi ya TSC Kilosa tarehe 11/08/2023.*

# TSC YATAKIWA KUENDELEA KUUTANGAZA MFUMO WA TSCMIS ILI WALIMU WAWEZE KUUTUMIA

**Na Mwandishi wetu – Mbeya**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetakiwa kuendelea kuutangaza mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) ili walimu wote wa shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma waweze kuutumia.

Hayo yalisemwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Sospeter Mtwale alipotembelea Banda la TSC katika Maonesho ya Wakulima Nanenane Kitaifa yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.

Mtwale alisema kwa kuwa mfumo huo umelenga kurahisisha huduma kwa walimu, kuna umuhimu wa TSC kuendelea kutumia njia mbalimbali za kufikisha elimu kwa walimu ili waweze kujiunga na kutumia mfumo huo kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za kiutumishi.

"Kwanza, nimefurahishwa sana na kukamilika kwa mfumo huu kwani utamaliza malamiko mengi ya walimu, sasa tunauhakika kuwa mwalimu akituma hoja yake itafanyiwa kazi kwa haraka na atapata mrejesho. Pili, ninawapongeza kwa jitihada zenu mnazofanya katika kuhakikisha kuwa mfumo huu unafahamika kwa walimu. Endeleeni na juhudi hizi ili mhakikishe kila mwalimu anayepaswa kutumia mfumo huu anautumia ili tumalize changamoto zao kwa haraka zaidi," alisema Mtwale.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema TSC kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imekamilisha kutengeneza Mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information system (TSCMIS) toleo la 1.0.0 wenye lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume katika kuwahudumia walimu.

"Mfumo huu umelenga kuwaondolea walimu usumbufu wa kufuata huduma kwenye Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya na Makao Makuu badala yake mwalimu atakuwa na uwezo wa kuingia kwenye Mfumo mahali popote kwa kutumia Kishikwambi alichopatiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwasilisha suala au lalamiko kuhusu utumishi wake.

Aliongeza kuwa, "kama mwalimu atakuwa na hoja zake, ataingia kwenye mfumo atatoa taarifa ataweka hoja yake na atatuma. Akishatuma ana uwezo wa kufuatilia na kuona hoja yake ilipofikia na pale itakapokuwa imejibiwa atapata majibu hapo hapo. Hivyo, kwa kupitia simu ya mkononi mwalimu atapata huduma zote za kiutumishi."



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Sospeter Mtwale akizungumza na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (aliyeshika kitabu) pamoja na watumishi wengine wa TSC waliokuwa wanatoa huduma kwenye banda la Tume hiyo wakati wa maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya.*





*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa ufafanuzi kwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Sospeter Mtwale wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa na Kimataifa mapema mwezi Agosti, 2023 mkoani Mbeya.*

*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akikabidhi Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Sospeter Mtwale wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa na Kimataifa mapema mwezi Agosti, 2023 mkoani Mbeya.*





*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Sospeter Mtwale akisaini kitabu cha wageni kwenye banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya.*



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Sospeter Mtwale (wa nne kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kulia) pamoja na watumishi wa TSC waliokuwa walioshiriki maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya.*

Watumishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi zake walioshiriki Maonesho ya Nanenane Kanda ya Kati yaliyofanyika mkoani Dodoma wakiwa katika maonesho hayo.














# MKURUGENZI IDARA YA AJIRA MAADILI NA MAENDELEO YA WALIMU WA TSC AFANYA ZIARA MKOANI TABORA

**Na Mwandishi wetu – Dodoma**



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Fatuma Muya akiambatana na watumishi wengine wa TSC, Francis Ngwankisa na Stella Njau wamefanya ziara ya ufuatiliaji wa majukumu ya Tume katika Wilaya tatu (3) za Mkoa wa Tabora amabazo ni Tabora, Sikonge na Urambo.

Ziara hiyo iliyofanyika tarehe 20 hadi 24 Agosti, 2023 ililenga kuona/kubaini endapo majukumu ya Tume kwa Mujibu wa Kifungu cha 5 (a) - (l) na Majukumu ya Tume ngazi ya Wilaya Kifungu cha 12(1) (a) – (h) vya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura Na. 448 yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyotolewa ikiwa ni pamoja na kuona changamoto na mafanikio yaliyopo katika kutekeleza majukumu hayo.

Kwa mujibu wa taarifa ya ziara hiyo, kwa nyakati tofauti Timu ya ufuatiliaji ilipata fursa ya kukutana Makatibu Tawala wa Wilaya za Tabora na Sikonge pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ambapo Mwl. Muya aliwaeleza namna TSC inavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria huku akiwaomba viongozi hao kuendelea kushirikiana na TSC ili kumaliza kero na malalamiko ya walimu.

Aidha, Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu alimshukuru Mkurugenzi wa Wilaya ya Sikonge kwa kuipatia Tume ofisi katika jengo jipya la Halmshauri ya Wilaya ya Sikonge na ushirikiano wake unaoleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Tume ikiwemo masuala ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu kwa ujumla.

Vilevile, Timu hiyo ilipata fursa ya kukaa na watumishi wa TSC wa Wilaya hizo na kuwapatia elimu juu ya masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kuhudumia walimu.








*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongea na watumishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI alipotembelea banda la ofisi hiyo Agosti 7, 2023 kwenye maonesho ya Nanenane mkoani Mbeya.*

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama ametoa wito kwa Maafisa wa TAMISEMI na Taasisi zake kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mwl. Paulina amesema hayo tarehe 7 Agosti, 2023 alipotembelea katika Banda la Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi zake wakati wa Maonesho ya Wakulima NaneNane Kitaifa yaliyofanyika Agosti 1 – 8, 2023 katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.

Amesema TAMISEMI ni Wizara pekee inayotekeleza shughuli za Serikali kwa wananchi wake moja kwa moja katika Jamii.

Amesema ni wajibu wa Maafisa waliopo katika maonesho hayo kutoa elimu lakini pia kusikiliza kero na changamoto wananchi wanazozisema kwa kutoa ufafanuzi na zile za kufanyiwa kazi ni vyema kuzipeleka katika Mamlaka ili ziweze kushughulikiwa.

Alieleza kuwa lengo la TAMISEMI na Taasisi zake kuwepo kwenye maonesho hayo ni kuwapa nafasi wananchi kupata huduma kwa urahisi kwa kukutana na watoa moja kwa moja.

Hivyo, ametoa wito kwa Maafisa wa Taasisi zote zinazosimamiwa na TAMISEMI kuhakikisha wanawagusa wananchi kwa utoaji wa huduma bora.

Maonesho ya Wakulima ya mwaka 2023 yalibeba kauli mbiu, "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula."



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisaini Kitabu cha wageni alipotembelea banda la Ofisi ya Rais TAMISEMI wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Agosti 1 – 8, 2023 katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwaongea na mhudumu katika moja ya mabanda ya Ofisi ya Rais TAMISEMI wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika tarehe 1 – 8 Agosti, 2023 katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.*

# KATIBU TSC AFANYA ZIARA KATIKA OFISI YA TSC GAIRO, AHIMIZA USAMBAZAJI WA KITABU CHA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI NA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU

**Na Mwandishi Wetu – Gairo**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama tarehe 10 Agosti, 2023 amefanya ziara katika ofisi za TSC Wilaya ya Gairo ambapo amewahiza watendaji wa ofisi hiyo kukamilisha zoezi la usambazaji wa nakala za Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kwa Wakuu wa Shule za Msingi za Wilaya hiyo.

Katika ziara hiyo, Watendaji wa TSC Wilaya ya Gairo walimueleza Katibu huyo kuwa wamegawa nakala za kitabu hicho katika kata 12 kati ya 18 na zoezi linaendelea.

Akitoa maelezo kwa Katibu wa TSC, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Gairo, Juma Eustace alisema miongoni mwa changamoto zinazoikabili ofisi hiyo ni Jiographia ya kuzifikia baadhi ya shule, vyombo vya usafiri pamoja na upungufu/uchakavu wa vitendea kazi.

Katibu wa Tume alitoa ufafanuzi wa namna ya kuzitatua changamoto hizo ikiwemo ununuzi wa kompyuta mpakato (laptop) kupitia mradi wa BOOST ambapo Ofisi ya TSC Wilaya ya Gairo itakuwa miongoni mwa wanufaika; kuendelea kushirikiana na Idara zingine ndani ya Halmashauri na kutumia vyombo vya usafiri vilivyopo kwa sasa kuzifikia shule.

Vilevile, Katibu huyo alisisitiza matumizi ya mfumo wa TSCMIS katika kushugulikia malalamiko, kero na changamoto za walimu ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao, kuongeza uwazi na tija, na kutoa huduma stahiki kwa walimu na kwa wakati.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika kikao na watendaji wa TSC Gairo tarehe 10 Agosti, 2023.*

Aidha, Nkwama alipata fursa ya kusalimiana na Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Mhe. Jabari Omary Makame na kumweleza jinsi ambavyo TSC imejipanga kuondoa malalamiko, changamoto na kero za walimu kwa kutumia mfumo wa TSCMIS ambapo Mhe. Makame aliipongeza TSC kwa hatua hiyo na kuishauri Tume hiyo kutoa mrejesho kwa walimu watakaowasilisha hoja zao katika mfumo huo.

Vilevile, Mhe. Makame alimueleza Katibu huyo jinsi Wilaya ya Gairo inavyotekeleza KPIs na kueleza kuwa katika wilaya hiyo Elimu ni ajenda ya kudumu kwa watendaji pamoja na madiwani.

"Baadhi ya KPIs za waheshimiwa Madiwani ni kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoto wakiwemo wenye mahitaji maalumu wakati wa kwenda na kurudi kutoka shuleni, upatikanaji wa chakula cha mchana shuleni, kusimamia uandikishaji na udahili wa wanafunzi na kudhibiti utoro wa wanafunzi shuleni, kusimamia ujenzi wa miundombinu ya shule, kuwasimamia wazazi kushiriki kikamilifu katika kufuatilia maendeleo ya kielimu ya watoto wao shuleni, na kusimamia ipasavyo afua za utekelezaji wa elimu katika kata wanazoziongoza na kutoa mrejesho kwa wananchi," alisema Mhe. Makame.

Akiwa wilayani hapo, Mwl. Nkwama alifika Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kabla ya kuendelea na ziara katika ofisi za TSC katika Mkoa wa Morogoro.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Gairo tarehe 10 Agosti, 2023.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akizungumza na Mkuu wa Wilaya Gairo, Mhe. Jabari Omary Makame tarehe 10 Agosti, 2023.*















*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa huduma kwa wateja waliotembelea banda la TSC tarehe 7 Julai, 2023 katika maonesho ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya*










*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongea na wanafunzi waliotembelea banda la TSC tarehe 7 Julai, 2023 katika maonesho ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.*

*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi waliotebelea banda la TSC tarehe 7 Julai, 2023 katika maonesho ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.*




*Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Festo Dugange akiongea na waandishi wa habari nje ya banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 5 Agosti, 2023 katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya. Naibu Waziri huyo ametembelea Mabanda ya Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Taasisi zake.*










*Wanafunzi wakipata maelezo katika banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 5 Agosti, 2023 katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.*







*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika mahojiano na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa na Kimataifa mkoani Mbeya hivi karibuni.*




*Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Fatuma Muya akiwa katika mahojiano na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa na Kimataifa mkoani Mbeya hivi karibuni.*

# DKT. MSONDE AKABIDHI BENDERA KWA TIMU YA TANZANIA INAYOSHIRIKI MASHINDANO YA FEASSSA NCHINI RWANDA

**Na. Mwandishi Wetu – Rusumo.**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Elimu), Dkt. Charles Msonde amekabidhi bendera ya Tanzania kwa Timu za Wanafunzi, Walimu na Viongozi wanaoenda kushiriki katika Mashindano ya 21 ya Michezo ya Shule za Msingi na Sekondari ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (FEASSSA) yaliyofanyika nchini Rwanda.

Makabidhiano hayo yalifanyika Agosti 17, 2023 katika Shule ya Sekondari Rusumo Wilayani Ngara Mkoani Kagera wakati msafara wa timu hizo ukielekea nchini Rwanda.

Akizungumza na Wanafunzi, Walimu na Viongozi wanaoenda kushiriki Mashindano hayo, Dkt. Msonde aliwata kila mmoja wao kuhakikisha anajituma na kutumia umahiri kwa kila mchezo huku wakitambua kuwa wanaliwakilisha Taifa la Tanzania katika mashindano hayo.



Aidha, Dkt. Msonde alisisitiza upendo, umoja na mshikamano kwa washiriki wote ambao wataungana nao katika Mashindano ya FEASSA ambayo yanashirikisha nchi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Rwanda, Kenya na Uganda.

Mashindano hayo yalianza Agosti 17, 2023 na yatafikia kilele Agosti 27, 2023 ambapo Tanzania inashiriki katika michezo ya Soka, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Wavu, Hockey, Tennis, Riadha, Mpira wa Mikono na Mpira wa Pete (Netboli).

# WIZARA ZA ELIMU NA TAMISEMI ZAPOKEA MAHITAJI YA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU NA MITAALA PENDEKEZWA

**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.**

Mawaziri; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof Adolf Mkenda na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, hivi karibuni wamekutana Jijini Dar Es Salaam na Kamati mbili za Kitaifa za Sera ya Elimu na Maboresho ya Mitaala kwa lengo la kupokea wasilisho la Mahitaji ya Utekelezaji wa Sera na Mitaala ya Elimu pendekezwa.

Wasilisho la pamoja lilifanywa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maboresho ya Mitaala, Prof. Makenya Maboko, aliyewasilisha juu ya Mahitaji Muhimu katika Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mitaala pendekezwa.

Mawaziri hao kwa pamoja wameweza kupokea mapendekezo hayo na kutoa maelekezo mbalimbali ya kufanyiwa kazi kwa ajili ya kuboresha mapendekezo hayo kabla ya kupelekwa kwenye Mamlaka za Maamuzi.

Kikao hicho pia, kilihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Elimu), Dkt. Charles Msonde na Mwenyekiti wa Kamati ya Sera, Prof. Joseph Semboja.

Wengine waliohudhuria ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Aneth Komba, pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya TET na Wajumbe wa Kamati ya Sera.


OFISI YA RAIS
TAMISEMI
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WATOTO WA MAMA SAMIA
#TAMISEMI Michezo
MASHINDANO YA FEASSSA YAHITIMISHWA RASMI NCHINI RWANDA
27.08.2023


OFISI YA RAIS
TAMISEMI
#TAMISEMI Michezo
WATOTO WA MAMA SAMIA TUMERUDI NA USHINDI - MASHINDANO YA FEASSSA
27.08.2023


OFISI YA RAIS
TAMISEMI


OFISI YA RAIS
TAMISEMI


#TAMISEMI Michezo


OFISI YA RAIS
TAMISEMI
#TAMISEMI Michezo
BENDERA YA TANZANIA IMEPEPERUSHWA VYEMA MASHINDANO YA FEASSSA
27.08.2023


OFISI YA RAIS
TAMISEMI
#TAMISEMI Michezo


OFISI YA RAIS
TAMISEMI
#TAMISEMI Michezo

# WAKUU WA MIKOA WATAKIWA KUKAMILISHA AHADI KUPATA FEDHA ZA GPE



**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.**

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ametoa wito kwa Wakuu wa Mikoa walioahidi kutoa zaidi ya Shilingi Bilioni 465 kama ahadi ambazo zitaisaidia nchi kupata fedha za ruzuku (grant) kiasi cha Dola milioni 50.

Mheshimiwa Jakaya Kikwete ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi iliyo chini ya Taasisi ya Ushirikiano wa Elimu Duniani (Global Partnership for Education) aliyasema hayo tarehe 31.08.2023 Jijini Dar es Salaam wakati akitoa hotuba yake kama mgeni rasmi katika hafla iliyohudhuriwa na Wakuu wa Mikoa na Wadau wa Elimu kutoka mikoa yote Tanzania Bara.

“Tumeshasikia jinsi ahadi zilivyotolewa, zaidi ya shilingi Bilioni 465, matumaini yangu walioahidi watatoa, ahadi ni deni, Wakuu wa Mikoa mmetoa ahadi wenyewe hapa” amesema Mheshimiwa Jakaya Kikwete.

Aidha, Kikwete alisema miradi ya GPE nchini, ilifadhiliwa kwa awamu mbili za mwaka 2014 hadi 2018 na 2018 hadi 2023 ikihusisha ujenzi wa madarasa mapya ya shule za msingi 2,980, mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalum 14, matundu ya vyoo 7,673, shule mpya 98, shule mpya 18, nyumba za walimu 94, ukarabati wa vituo vya walimu 13 (TRC), ujenzi na uendeshaji wa vituo vya walimu 12, uendeshaji wa Mafunzo ya Walimu Kazini (MEWAKA) na ununuzi wa vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia kwa walimu na wanafunzi.

Kwa upande wake Prof. Adolf Mkenda akimkaribisha mgeni rasmi alisema Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga imani kubwa kwa Sekta Binafsi nchini na ndio maana Wadau wameitikia kwa kiwango kikubwa na kuendelea kutoa michango yao kwenye elimu hapa nchini na hivyo ni jambo jema kwa wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI kutambua mchango wa Wadau kwenye Sekta ya Elimu nchini.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI Adolf Ndunguru alitoa rai kwa Wakuu wa Mikoa kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa utekelezaji wa ahadi zilizowekwa na Wadau, kuanzisha ‘Kanzidata’ kwa kila mkoa ili kurahisisha ufuatiliaji na tathmini ya ahadi zilizotolewa lakini pia kuendelea kuwaelimisha Wadau kwa kuwa zoezi hilo ni endelevu.

Mpaka sasa Washirika wa GPE Duniani wanatoa msaada wa kifedha kwa nchi 88 ili kuinua Sekta ya elimu na kutimiza lengo la kutomuacha nyuma mtoto yeyote katika kupata haki ya elimu.

Katika ahadi zilizotolewa mkoa wa Mara umeibuka kidedea kwa kutoa ahadi ya Shilingi Bilioni 155 wakati Dar es Salaam ukiahidi kutoa Shilingi Bilioni 20.



# MILIONI 331 YAJENGA MADARASA KUONDOA MSONGAMANO WA WANAFUNZI SHULE YA MSINGI MAMBAMBA

- Mama Samia atoa fedha hiyo kupitia Mradi wa BOOST kujenga madarasa;
- Zaidi ya bilioni 230 kujenga shule mpya na madarasa nchi nzima;
- Tandahimba yapokea Milioni 95 Ujenzi wa Nyumba za Walimu Shule za Msingi na Milioni 95 Ujenzi wa Nyumba za Walimu Shule za Sekondari; na
- TARURA kukarabati Kilomita 7.2 barabara kutoka Mambamba, Mwimbi hadi Tandahimba kupitika majira yote.

**Na. Mwandishi Wetu – Tandahimba.**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Deogratius Ndejembi amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa Shilingi Milioni 331 kupitia Mradi wa BOOST zilizojenga madarasa yatakayotatua changamoto ya msongamano wa Wanafunzi katika Shule ya Msingi ya Mambamba 'B' Wilayani Tandahimba.

Mhe. Ndejembi alisema hayo akiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, mara baada ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, kumpatia fursa ya kuzungumza na wakazi wa eneo hilo.

Mhe. Ndejembi alifafanua kuwa, Rais wa Awamu ya Sita, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitafuta zaidi ya bilioni 230 kwa ajili ya kujenga shule mpya na madarasa nchi nzima kupitia Mradi wa BOOST kwenye maeneo ambayo shule zina msongamano wa wanafunzi au hakuna shule kabisa, ambapo Tandahimba imenufaika na ujenzi wa Shule ya Msingi ya Mambamba 'B' iliyogharimu shilingi Milioni 331.

"Mhe. Waziri Mkuu Milioni 331 imejenga madarasa haya mazuri yenye kupendeza katika Shule hii ya Msingi ya Mambamba 'B' ambayo yatasaidia kutatua changamoto ya msongamano wa wanafunzi uliopo katika Shule Mama ya Mambamba, ikiwa ni pamoja na kuwaondolea adha wanafunzi kutembea umbali mrefu." Mhe. Ndejembi alisisitiza.

Aliongeza kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilipokea Milioni 95 kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba za Walimu wa Shule ya Msingi na Milioni 95 nyingine kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba za Walimu wa Shule za Sekondari.

Aidha, Mhe. Ndejembi alisema TARURA imetenga fedha kwa ajili ya kukarabati barabara ya Kilomita 7.2 ya kutoka Mambamba kwenda Mwimbi hadi Tandahimba ili iweze kupitika katika majira yote.

# MTWALE AHIMIZA KUKAMILISHWA KWA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU YA AWALI, MSINGI NA SEKONDARI

**Na. Mwandishi Wetu – Geita.**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Sospeter Mtwale, ameuhimiza Uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Geita kuhakikisha miundombinu ya elimu inayojengwa kwenye Shule za Awali, Msingi na Sekondari kupitia fedha za BOOST, Serikali Kuu na BARICK inakamilika kwa wakati ili wanafunzi wanufaike kitaaluma.

Bw. Mtwale alitoa wito huo hivi karibuni kwa Uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, wakati akiwa katika ziara yake ya kikazi iliyolenga kuhimiza uwajibikaji na kukagua miundombinu ya elimu inayojengwa na Serikali katika Halmashauri hiyo.

Bw. Mtwale alisisitiza upanuzi wa miundombinu katika shule za sekondari kidato cha tano kupitia fedha za Serikali Kuu, ukamilike kwa wakati kwa kuzingatia ubora na thamani ya fedha iliyotolewa.

Sanjali na hilo, Naibu Katibu Mkuu huyo alielekeza majengo ambayo bado yapo katika hatua za awali za ujenzi yaongezewe idadi ya mafundi wenye uwezo ambao watafanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ujenzi kwa wakati.

Aliongeza kuwa, mafundi hao wanapaswa kusimamiwa katika hatua zote, hususani kwenye hatua ya ukamilishaji ili kupata majengo yenye ubora na yanaoendana na thamani ya fedha iliyotumika.

# NDEJEMBI ASHIRIKIANA NA WANANCHI KUCHIMBA MSINGI WA SHULE ZINAZOJENGWA KATA YA MANCHALI CHAMWINO

**Na. Mwandishi Wetu – Chamwino.**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi, ameshirikiana na wananchi wa Kata ya Manchali kuchimba msingi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Manchali itakayoitwa Ndejembi pamoja na Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Dodoma inayojengwa katika kata hiyo kupitia mradi wa SEQUIP.

Mhe. Ndejembi alisema, Wananchi wa Kata ya Manchali wanashiriki kikamilifu katika ujenzi wa shule hizo ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuboresha elimu nchini.

Mhe. Ndejembi alifafanua kuwa, ushiriki wa wananchi unapunguza gharama za ujenzi na kuongeza kuwa lengo lake ni kuhakikisha Shule ya Sekondari ya Ndejembi inakamilika na fedha inabaki, ikizingatiwa kuwa wananchi wamempa heshima kwa kuipa shule hiyo jina lake kwa kuthamini mchango wake.

Akizungumzia jitihada za kupunguza gharama ya ujenzi katika Shule ya Sekondari ya Wasichana inayojengwa, Mhe. Ndejembi alisema Uongozi wa Halmashauri umemtafuta mzabuni wa kufyatua tofali ambaye amefungua kiwanda cha kufyatua tofali kwa gharama nafuu ya shilingi 1,400 kwa tofali kwenye eneo ambalo shule hiyo inajengwa.

Aidha, Mhe. Ndejembi alimshukuru Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha za kujenga wa shule hizo katika Kata ya Manchali, shule ambazo zitatatua changamoto ya wanafunzi wa eneo hilo na maeneo jirani kutembea umbali mrefu ili kupata elimu.

"Rais Samia tangu aingie madarakani amefanya mambo makubwa kwa Wananchi wa Jimbo la Chamwino kwani kila eneo ametoa fedha za ujenzi wa miundombinu ya elimu kwa ajili ya kutatua changamoto ya wanafunzi kutembea umbali mrefu." Mhe. Ndejembi alisisitiza.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu (Elimu), Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Dkt. Charles Msonde, aliwapongeza Wananchi wa Manchali kwa kushiriki kikamilifu kuchimba msingi wa shule za sekondari zinazojengwa na kuongeza kuwa, ushiriki wao ni ishara ya kuunga mkono kwa vitendo jitihada za Mheshimiwa Rais kuboresha elimu nchini.



# PELEKENI WATOTO SHULE MIUNDOMBINU IPO TAYARI - DKT. MSONDE

**Na. Mwandishi Wetu – Chamwino.**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde, amewataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawapeleka shuleni watoto waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka 2023 kwa kuwa mioundombinu imekamilika.

Dkt. Msonde alitoa tamko hilo hivi karibuni mara baada ya kukagua miundombinu ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha tano katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Alisema wanafunzi 130,446 wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano kwenye Shule 548 kwa mwaka 2023 na kati ya hao Wanafunzi wa bweni ni 125,402 na Wanafunzi 5,044 ni wanafunzi wa kutwa.

Dkt. Msonde alisema kumekuwa na ongezeko la Wanafunzi, hivyo kupelekea Serikali kutoa fedha za kuongeza miundombinu ya mabweni ili kuwapokea wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano na kuwataka wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao wanaripoti shuleni ifikapo Agosti 13, 2023 kwa ajili ya kuanza masomo.

"Niwatake wazazi na walezi kuhakikisha watoto wetu waliopangiwa kidato cha tano wanaripoti katika Shule walizopangiwa kwa wakati ili waanze masomo kwa wakati tena kwa pamoja ili wasipishane katika masomo." Alisisitiza Dkt. Msonde.

Kuhusu wanafunzi walioomba kuhamia shule nyingine, Dkt Msonde alisema Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepokea maombi hayo na kuwataka wanafunzi hao kwenda kuripoti katika shule walizopangiwa kwa sasa.

"Maombi tumeyapokea ila tutayashughulikia wakati wanafunzi wakiwa shule pindi nafasi zinazopatikana kama kuna wanafunzi watakwenda shule binafsi." Alisema Dkt. Msonde.

Aidha, Dkt. Msonde aliwataka Wakuu wa Shule kuwabadilishia tahasusi wanafunzi walioomba kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

"Lakini kwa Mwanafunzi anayeomba kubadili tahasusi ambayo haipo kwenye shule aliyochaguliwa anapaswa kuandika barua kwenda kwa Katibu Mkuu, OR – TAMISEMI, ili kupelekwa katika Shule husika kama nafasi ikitokea ndani ya miezi miwili." Alisema Naibu Katibu Mkuu huyo.

Kadhalika, aliwataka Walimu kuhakikisha wanawapokea watoto na kuwa nao karibu kimalezi na kujiepusha kuwatoza michango ambayo haijaelekezwa na Serikali.

"Kama ni Sare ya Shule tumwambie ni ya rangi gani, na kama ni kiatu tumwambie cha aina gani, kama rimu ya karatasi basi tumwambie ni karatasi gani. Mtoto aje na kitu hicho na tusimwambie leta fedha ili tusiingie pia kwenye msuguano na malalamiko yasiyo ya lazima." Alisema.

Awali, Afisa Elimu Mkoa wa Dodoma, Gifti Kyando, aliishukuru Serikali kwa uamuzi wa kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha na kujenga miundombinu mipya katika Shule za Sekondari hasa zile ambazo zinawapokea wanafunzi wa kidato cha tano mwaka 2023.



**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**

# TAMISEMI MSHINDI WA PILI NANENANE KANDA YA KATI

Ofis ya Rais - TAMISEMI imeibuka Mshindi wa Pili katika Kundi la Wizara za Serikali kwenye Maonesho ya Nanenane Kanda ya Kati, Nzuguni - Jijini Dodoma ambayo yalifikia tamati Agosti 08, 2023.

Maonesho hayo ya Nanenane yalihitimishwa Agosti 08, 2023 ambapo Ofisi ya Rais imefanikiwa kupata cheti kilichopokelewa na Mratibu wa Maonesho wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa Kanda ya Kati, Bi. Hoffu Mwakaja.

Maonesho hayo yalihitimishwa na Mhe. Patrobas Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na kusema Serikali inatambua mchango wa Wakulima na ndio maana inaweka mipango thabiti ya kilimo kuwa endelevu na kukifanya kuongeza wigo wa ajira ikiwa ni pamoja na kuongeza Bajeti ya Kilimo inayokaribia shilingi Trilioni moja kwenye Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Katambi alisema Serikali inaendelea kutatua changamoto za kilimo kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo na mifugo, kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, huduma za ugani, kujenga miundominu ya mifugo, kufanya utafiti wa kilimo na mifugo pamoja na kuendesha kilimo cha kiteknolojia.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akitoa salamu za utangulizi alimshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kufanya Maonesho ya Kanda ya Kati kuwa endelevu badala ya kusubiri kipindi cha mwezi Agosti ya kila mwaka kwani itainua pato la Mkulima na Mfugaji.

Kwa upande wake Peter Serukamba, Mkuu wa Mkoa wa Singida, akitoa neno la awali alisema Wakulima wa Kanda ya Kati walipata fursa ya kuhudhuria Makongamano ya Mazao ya Mtama na Alizeti lakini pia Wafugaji walipata fursa ya Shindano la Nyama Choma na Paredi ya Mifugo ambayo itasaidia kuongeza thamani ya mazao ya Mifugo na Kilimo na kuwaongezea uzoefu.

Mgeni Rasmi Mhe. Patrobas Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu alipata fursa ya kutembelea mabanda ya maonesho likiwemo Banda la Halmashauri ya Wilaya ya Singida na kujionea Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Kilimo na Mifugo pamoja na vikundi vilivyojipatia fedha za mikopo ya asilimia 10 vinavyofanya shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo.



# WADAU WA ELIMU WAOMBWA KUSHIRIKI KUCHANGIA MAENDELEO YA ELIMU NCHINI

**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, amewaomba Wadau wa Maendeleo nchini kushiriki katika kuchangia Maendeleo ya Elimu kwa kutoa kiasi cha fedha kitakachoiwezesha Serikali kukidhi kigezo cha kupata ufadhili wa zaidi ya dola za Marekani milioni 50 kupitia Multplier Grant 2023.

Mhe. Kairuki alitoa ombi hilo kwa Wadau wa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam Agosti 14, 2023 katika Ukumbi wa Anatouglo Jijini Dar es Salaam kwenye Kikao Kazi kilicholenga kuwajengea uelewa kuhusu dhana ya GPE LANES MULTIPLIER GRANT na kuwashawishi kuchangia Maendeleo ya Elimu Msingi.

Mhe. Kairuki alisema endapo Tanzania itaweza kupata ufadhili huo, fedha zake zitachangia katika kuiwezesha Serikali kutekeleza mipango mipya endelevu iliyoibuliwa na mabadiliko ya Sera na Mitaala ya Elimu hususani katika kufanikisha utekelezaji wa eneo la Mafunzo ya Amali.

Alisema kuwa kupitia ufadhili wa GPE Multiplier nchi 18 zimetengewa dola za Marekani milioni 50 kiwango cha juu cha mgao ‘Maximum Allocation’ kwa Mwaka 2023 ambapo Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo lakini fedha hizo zitatolewa kama nchi itakidhi kigezo cha wadau elimu nchini kuchangia.

Mhe. Kairuki alisema upatikanaji wa motisha hiyo unafuata hatua mbalimbali ambapo kila dola moja ya Marekani itakayotolewa kupitia Sekta Binafsi ikiwemo Kampuni, Asasi za Kiraia na Benki, Mfuko wa GPE utatoa dola moja ya Marekani.

Alisema kuwa kila dola tatu za Marekani zitakazotolewa kama msaada au msamaha wa fedha za mkopo kutoka katika Taasisi za Fedha za Kimataifa au Nchi Washirika wa Maendeleo, Mfuko wa GPE utatoa dola moja ya Marekani hivyo amewaomba Wadau wa Maendeleo ya Elimu nchini kuchangia fedha.

“GPE wameonesha nia ya kutufadhili kiasi cha dola za Marekani milioni 50 baada ya wadau wa ndani kuonyesha nia ya kuchangia katika masuala ya elimu msingi, ninawaomba sana wadau wetu kuiwezesha nchi kupata fedha hiyo itakayotumika kuboresha miundombinu ikizingatiwa kuwa bado kuna uhitaji mkubwa.” Mhe. Kairuki alisisitiza.

Aidha, Mhe. Kairuki alisema kuwa ili kuweza kupata fedha kupitia ufadhili wa GPE Multiplier, wadau watatakiwa kuandika barua za kuweka nia ya kuchangia katika masuala ya elimu msingi ili kuwezesha nchi kujaza tamko la nia za wadau kuchangia kupitia Fomu ya “Expression of Interest (EoI) itakayotumika kama kigezo cha upatikanaji wa ufadhili huo.



# WALIMU WATAKIWA KUWA CHACHU YA MABADILIKO MATUMIZI YA TEHAMA SHULENI

**Na. Mwandishi Wetu – Tabora.**

Serikali imeeleza kuwa katika Zama za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji ni nyenzo muhimu itakayorahisisha utoaji wa elimu bora kwa ufanisi nchini.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Bw. Eprahim Simbeye, kwenye Mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu wa Shule za Awali na Msingi Tanzania Bara yaliyofanyika katika Chuo cha Ualimu Tabora, Mkoani Tabora.

Simbeye alieleza kuwa kumekuwa na matumizi makubwa ya TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji hivyo ni muhimu kwa Walimu kuendana na mabadiliko hayo ili kuendana na malengo ya Serikali ya kutoka Elimu Bora na kwenda na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia yanayoendelea duniani.

"Matumizi ya TEHAMA ni muhimu kwa sasa, matumizi ya karatasi na kuandika vinapotea, hivyo ni muhimu kupata ujuzi na maarifa kuhusu matumizi sahihi ya vifaa vya TEHAMA katika Ujifunzaji na Ufundishaji nchini." Alisema Simbeye.

Alisema kuwa ni Wajibu wa kila Mwalimu kutumia vifaa walivyonavyo katika Ufundishaji na Ujifunzaji hasa matumizi sahihi ya vishikwambi pamoja na kompyuta kwa ajili ya kufundisha ili kuendana na mabadiliko ya teknolijia.

"Tumieni vishikwambi mlivyopatiwa na Serikali kwa ajili ya kufundisha na kupata maarifa badala ya kuvitumia kinyume na utaratibu." Alisisitiza Simbeye.

Aliwataka Walimu hao kuhakikisha wanaitendea haki kada yao katika kuhakikisha wanatumia ujuzi walioupata katika kuwafundisha wengine juu ya matumizi sahihi ya vifaa vya TEHAMA shuleni.

Simbeye aliwataka Walimu hao kuhakikisha wanakuwa chachu ya mabadiliko kwenye vituo vyao vya kazi kwa kuhakikisha wanafundisha na kusimamia maadili bora kwa Wanafunzi ili kujenga Taifa lenye Maadili.

Mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya vifaa vya TEHAMA na vishikwambi katika kufundisha na kujifunza kwa Walimu wa Shule za Awali yanasimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolijia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia Mradi wa Kuimarisha na Kuboresha Utoaji wa Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara (BOOST).



# KAMATI YA LAAC YAPONGEZA USIMAMIZI NA MATUMIZI MAZURI YA FEDHA UJENZI WA SHULE MPYA MOLETI- KONGWA

**Na. Mwandishi Wetu – Kongwa.**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeupongeza Uongozi wa Kijiji cha Moleti Kata ya Chiwe, Halmashauri ya Kongwa kwa usimamizi na matumizi ya fedha iliyopelekwa kwa ajili ya ujenzi wa Shule Mpya ya Msingi kupitia Mradi wa BOOST.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Mhe. Stanslaus Mabula, alitoa pongezi hizo hivi karibuni kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati wakati wa ziara kijijini Moleti kukagua utekelezaji wa ujenzi wa shule mpya iliyojengwa kupitia Mradi wa BOOST uliogharimu shilingi milioni 318.

Mhe. Mabula alisema moja ya jukumu la Kamati yake ni kusimamia matumizi ya fedha zinazopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi zinatumika vizuri na matumizi yake yalingane na thamani ya fedha iliyotolewa kwenye mradi husika.

Akiongea kwa niaba ya Kamati, Mhe.Mabula aliridhishwa na usimamizi na matumizi ya fedha zilizotumika katika ujenzi wa miundombinu ya Shule Mpya ya Moleti yenye Vyumba saba (7) vya Madarasa, Vyoo vya Wanafunzi matundu nane (8), Vyoo vya Walimu matundu mawili (2), Vyumba viwili (2) vya Madarasa ya Mfano ya Wanafunzi wa Elimu ya Awali, Kichomea Taka, Jengo la Utawala na Utengenezaji wa Madawati kwa ajili ya Shule ya Msingi pamoja na meza na viti kwa ajili ya Wanafunzi wa Shule ya Awali.

Alitoa wito kwa Uongozi wa Kijiji kuendelea kushirikiana katika masuala ya maendeleo kijiji hapo kama walivyoshirikiana kwa kuhakikisha shule hiyo inakamilika kwa wakati na kuwataka kuwasimamia wanafunzi wasome ili wafikie malengo yao bila kuwakatisha masomo.

"Serikali inaleta miradi hii kwa ajili ya wananchi tuitunze, tuilinde lakini pia muhimu zaidi nasisitiza tuhimize watoto wetu wapate elimu, miundombinu hii ya shule imekamilika ni jukumu letu Wazazi na Walimu." Alisema Mhe. Mabula.

Awali akisoma taarifa ya ujenzi wa shule hiyo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Moleti, Mwl. Rose Justine, alisema shule hiyo imepunguza uhaba wa miundombinu na imesaidia kuboresha mazingira ya Ujifunzaji na Ufundishaji kutokana na mazingira yake kuwa mazuri.

Vilevile aliieleza Kamati ya LAAC kuwa kiasi cha fedha cha shilingi milioni 10 kilichobaki wameuomba Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa uridhie zitumike kwa ajili ya Uchimbaji wa Kisima cha Maji ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji jambo ambalo Kamati iliridhia.



# NDEJEMBI AELEKEZA KUREKEBISHWA KWA MADIRISHA YA SHULE MPYA YA MSINGI KONA NNE

**Na. Mwandishi Wetu – Ushetu.**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembi, amemtaka fundi aliyepewa kandarasi ya kujenga Shule Mpya ya Msingi ya Kona Nne iliyopo Halmashauri ya Wilaya Ushetu kurekebisha kwa gharama zake mwenyewe madirisha yote aliyoyaweka bila kuzingatia maelekezo ya Serikali.

Mhe. Ndejembi alimtaka fundi huyo kufanya marekebisho hayo haraka, wakati akikagua ujenzi wa miundombinu ya elimu katika Shule ya Mpya ya Msingi ya Kona Nne inayojengwa kupitia Mradi wa BOOST katika Kijiji cha Bugomba 'A', Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ambapo alibaini dosari kwenye madirisha ya 'aluminium' yaliyowekwa katika shule hiyo.

"Naelekeza ndani ya siku 14 madirisha yote yaondolewe ili marekebisho yafanyike kwa ufanisi tena kwa gharama za fundi na wasimamizi na sio kwa gharama za Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu." Mhe. Ndejembi alisisitiza.

Mhe. Ndejembi alisema amebaini madirisha hayo hayana wavu na hayajawekwa kwa viwango stahiki, hivyo marekebisho yafanyike na taarifa ya kukamilika kwa marekebisho hayo iwasilishwe kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Mkuu wa Wilaya ya Kahama na kwake ili kujiridhisha na utekelezaji wa maelekezo yake.

Aidha, alimtaka Kamanda wa TAKUKURU wa Wilaya ya Kahama kufanya Uchunguzi wa Matumizi ya Fedha katika ujenzi wa shule hiyo ili hatua za Kisheria zichukuliwe kwa watakaobanika kukwamisha jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita za kuboresha miundombinu ya elimu nchini.

Sanjari na hilo, alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Bi. Hadija Kabojela, kuchukua hatua za kinidhamu kwa Mwalimu Jonas Mabusi, ambaye ni Msimamizi wa Ujenzi na aliyekuwa Mkuu wa Shule hiyo, Bi. Stella Solezi, kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao ipaswavyo.



# PLAY MATTERS WATEMBELEA TAASISI YA ELIMU TANZANIA (TET)

**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es salaam.**

Shirika lisilo la Kiserikali Play Matters lililoanzishwa Mwaka, 2020 katika nchi za Uganda, Ethiopia na Tanzania kwa ajili ya Mpango wa Ufundishaji na Ujifunzaji kupitia Michezo Shuleni hivi karibuni limetembelea Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa lengo la kujifunza zaidi kuhusu Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA).

Akifungua kikao hicho kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa TET Jijini Dar Es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TET, Dkt. Aneth Komba, alisema kuwa, TET inashirikiana na Play Matters katika kuwapa Mafunzo Walimu waliopo kazini.

Aidha, alisema Shirika hilo limeandaa Matini yenye maudhui ambayo yatawasaidia kuwajengea uwezo walimu juu ya namna bora ya kutumia michezo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

"Kama mnavyojua, Serikali ya Awamu ya Sita inafanya mapitio makubwa ya mitaala na katika Rasimu za Mitaala tunazozipendekeza tumependekeza na kusisitiza matumizi makubwa ya michezo katika ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto. Hivyo, Play Matters wamekuja wakati muafaka na tutashirikiana nao ipaswavyo katika kuhakikisha kwamba hii mbinu ya kutumia michezo inawafikia Walimu wote na wanaweza kutumia vizuri kuwafanya Watoto waweze kujifunza. Naamini, njia hii ikitumiwa vizuri hatuwezi kupata mtoto anayefika Darasa la Pili akiwa hawezi kusoma, kuandika na kuhesabu." Alisema Dkt. Aneth.

Kwa upande wa Wawakilishi kutoka Wizara ya Elimu Uganda na Ethiopia, waliipongeza TET kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika kuhakikisha Walimu wote nchini wanapata Mafunzo Kazini kwa kutumia teknolojia ambayo ni njia rahisi kufikiwa na Walimu wote.

Awali, Mkuza Mtaala Bw. Onesmo Sedikia, aliwasilisha kwa Wageni hao jinsi Mfumo wa Learning Managent System (LMS) na Online Library unavyotumiwa na Walimu katika Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji ikiwa ni pamoja na kujiendeleza kitaaluma.

Wageni hao walitoka Wizara ya Elimu ya Uganda, Ethiopia, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais -TAMISEMI.



# SERIKALI YAAHIDI KUENDELEA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA ELIMU

**Na. Mwandishi Wetu – Mbogwe.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Jenista Mhagama (Mb) Peramiho, amesema Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI itajenga vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Muungano iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni katika Kijiji cha Namatuhi Kata ya Ndongosi Halmashauri ya Wilaya ya Songea wakati wa Uwekaji wa Jiwe la Msingi la Ujenzi wa vyumba viwili vya Madarasa vinavyomaliziwa kujengwa katika shule hiyo.

"Tunataka kufanya ukarabati wa madarasa na kujenga mengine ili Shule ya Msingi Muungano iwe miongoni mwa shule za mfano kwa kuwa na Miundombinu Bora ya Elimu." Alisema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera, Bunge na Uratibu.

Waziri Mhagama, ameelekeza Watendaji wa Halmashauri za Wilaya kuhakikisha hatua ya umaliziwaji wa ujenzi wa vyumba hivyo viwili vya madarasa uwe umekamilika ndani kipindi cha wiki mbili.

Akizungumzia kuhusu uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji, Waziri Mhagama amewaomba Wananchi wa Kijiji cha Namatuhi kuendelea kuhifadhi mazingira na kuepuka tabia ya ukataji wa miti.

Alisema chanzo cha maji cha Kitinginyi ndio chanzo pekee kilichobaki, hivyo kinapaswa kulindwa kwa kuepusha shughuli nyingine za kibinadamu zinazoweza kuharibu chanzo hicho cha maji.

"Tuendelee kutunza chanzo hicho cha maji kwa kupanda miti ili huduma ya maji iweze kunufaisha vijiji vingine vya Jirani." Alisema Waziri Mhagama.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Mwl. Neema Magembe, alisema gharama za ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa mpaka ujenzi ulipofikia jumla ya shlingi millioni 34 zimetumika.

Aliongeza kwa kusema kuwa halmashauri tayari imeshaweka fedha za umaliziaji wa vyumba hivyo vya madarasa kwa kuweka marumaru.

Awali, Diwani wa Kata ya Ndongosi, Mhe. Zakaria Mbilinyi, alimshukuru Waziri Mhagama kwa kutuma Mhandisi wa Maji ambaye alifanya utafiti na kugundua chanzo cha maji katika Kitongoji cha Muungano kilichopo katika Kijiji cha Namatuhi Kata ya Ndongosi.

"Wananchi wana matumaini makubwa kwamba watapata huduma ya maji safi na salama kwa afya, uhai na shughuli nyingine muhimu za kibinadamu." Alisema Mhe. Mbilinyi.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama (Mb) Peramiho akiweka jiwe la Msingi Katika shule ya Msingi Muungano iliyopo katika kijiji cha Namatuhi kata ya Ndongosi.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama (Mb) Peramiho akizungumza jambo na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Halmashauri ya Wilaya ya Songea Ndg. Thomas Simon Masolwa wakati wa mkutano wa hadhara Uliofanyika katika Kitongoji cha Muungano.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama (Mb) Peramiho akizungumza jambo Diwani wa Kata ya Ndongosi Mhe. Zakaria Mbilinyi wakati wa mkutano wa hadhara Uliofanyika katika Kitongoji cha Muungano.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama (Mb) Peramiho akicheza ngoma za kitamaduni na wakinamama wa kijiji cha Namatuhi wakati wa Ziara yake katika kata ya Ndongosi.*

# DKT. MSONDE AINGIA DARASANI KUFUNDISHA, KUPIMA UTEKELEZAJI WA KPI



**Na Mwandishi Wetu – Tabora.**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI (Elimu), Dkt. Charles Msonde akifundisha somo la hesabu wanafunzi wa darasa la Saba katika shule ya Msingi Ulaya iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga Mkoani Tabora.

Tarehe 28 Agosti 2023, Dkt. Msonde aliendelea na ziara ya kukagua hali ya utoaji wa elimu mashuleni na kukagua utekeleza wa vigezo vya kuboresha elimu nchini (KPI).

Aidha, Dkt. Msonde alitaka kujihakikishia utayari wa wanafunzi hao wa darasa la saba wanaotarajia kufanya mtihani wa kuhutimu elimu ya msingi mwezi Septemba 2023.













# VITABU VYA KIADA, BAADHI VYA ZIADA NA MACHAPISHO MBALIMBALI YA KIELIMU YAPATIKANA BURE KATIKA MAKTABA MTANDAO YA TAASISI YA ELIMU TANZANIA

**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es salaam.**

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inajivunia Matumizi ya Teknolojia kwa sasa ambapo Vitabu vyote vya Kiada, baadhi ya Vitabu vya Ziada na machapisho mengine mbalimbali yanapatikana katika Tovuti ya TET kupitia Maktaba Mtandao ambapo kwa sasa ni rahisi kwa mtu yoyote kuweza kuvipata na kusoma kwa urahisi.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mkuu wa TET, Dkt. Aneth Komba akiongea katika mahojiano maalumu na Vyombo vya Habari hivi karibuni katika Makao Makuu ya TET Jijini Dar es Salaam.

"Kwa sasa ukiwa na laini ya Airtel unaweza kuingia na kusoma bila kuwa na 'data (internet)' na tunaendelea kuzungumza na wadau wengine wa mitandao mbalimbali kuhakikisha machapisho yanapatikana bure ili kuwezesha usomaji kuwa rahisi kwa mtu yeyote atakayehitaji." Alisema Dkt. Komba.

Pia, alieleza kuwa kwa kiwango kikubwa teknolojia imesaidia katika upande wa Mafunzo ya Walimu Kazini kwa kutumia Mfumo Maalumu ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Walimu kupitia Jumuiya za Ujifunzaji ambapo katika mfumo huo zaidi ya Walimu 100,000 huingia kila siku na kuweza kuwasiliana na Wataalamu wa TET.

Aliongeza kuwa, Mfumo huo umeweza kupunguza gharama za kuwakusanya Walimu katika eneo moja kwa ajili ya kuwapa Mafunzo Kazini.



# WAZIRI SIMBACHAWENE APONGEZA NGUVU ZA WANANCHI KATIKA KUJENGA SHULE YA KISASA LUMUMA

**Na. Mwandishi Wetu – Kibakwe.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR – MUUUB) ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, Mhe. George Simbachawene, amewapongeza Wananchi wa Kata ya Lumuma kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kujenga Shule ya Sekondari ya Lumuma Green kwa nguvu zao wenyewe ambayo ina Wanafunzi 106 wa Kidato cha Kwanza kutoka Vijiji vitatu vinavyounda Kata hiyo.

Ametoa pongezi hizo wakati akizungumza na Wananchi kwa nyakati tofauti katika Vijiji vya Lufusi, Kitati na Lumuma Mafene katika Kata ya Lumuma kupitia Mikutano ya Hadhara aliyoifanya katika Vijiji vya Jimbo la Kibakwe.

Alisema amefurahishwa na uthubutu na utayari uliooneshwa na Wananchi wa Kata hiyo kwa kukubali kuunganisha nguvu zao kwa Pamoja katika kukamilisha shule hiyo yenye majengo ya kisasa.

Waziri Simbachawene aliesema Serikali inavutiwa na uongozi wenye maono na mtazamo wa kimapinduzi kwa kuanza kusaidia pale nguvu za Wananchi zilipoishia ili kuistawisha jamii hiyo.

Alimtaja Diwani wa Kata hiyo Mhe. Jocktan Cheligah, kama kiongozi mwenye maono, uthubutu na ubunifu ambaye amedhamiria kuhakikisha shule hiyo inajengwa ili Wanafunzi wa vijiji hivyo waweze kupata elimu katika mazingira rafiki.

Kufuatia hatua hiyo Mhe. Simbachawene aliahidi kusaidia kujenga nyumba pacha tatu kwa ajili ya kuwasaidia Walimu ambao wanaishi mbali na eneo la shule.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mbunge wa Kibakwe ambaye pia Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, Mhe. George Simbachawene akizungumza na Wananchi wa Kata ya Lumuma mara baada ya kutembelea shule iliyojengwa kwa nguvu za wananchi wa jimbo la Kibakwe mkoani Dodoma.*

Alisema akiwa ndiye Mbunge wa Jimbo lao la Kibakwe, anahitaji Wananchi wanaoonesha njia ili Serikali iweze kusaidia kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Kwa kujenga shule hii, mimi binafsi mmenitia moyo, hivyo naomba niwaahidi kuwa nitahakikisha hadi kufika mwakani tunakuwa na majengo mengi zaidi ili watoto wetu wasome katika mazingira bora." Alisisitiza Mhe. Simbachawene.

Alifafanua kuwa, nguvu za Wananchi zinahitajika ili kuhakikisha Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa kwani Serikali ina vipaumbele vingi hivyo bila Wananchi wenyewe kuanza kubuni miradi hiyo huwa ngumu kuitekeleza miradi hiyo kwa wakati.

Katika hatua nyingine Mhe. Simbachawene aliridhishwa na Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ulioibuliwa na Wananchi wa Kijiji cha Lufusi na kuahidi kuwa ataisaidia katika ukamilishaji wa zahanati hiyo kwa wakati.

"Naomba niwaahidi kuwa, kupitia Mfuko wa Jimbo na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa tutahakikisha fedha zinapatikana ili kusaidia katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa zahanati hiyo mliyoanza.

Naye, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Mhe. George Fuime, aliahidi kutenga fedha za kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili shule hiyo kwa nia ya kuunga mkono shughuli zinazofanywa na Wananchi wa Kata hiyo.

"Tutahakikisha fedha zinatengwa kwa ajili ya kuunga mkono nguvu za Wananchi katika masuala ya maendeleo yaliyobuniwa na Wananchi wenyewe." Alisema Mhe. Fuime.

Naye Diwani wa Kata hiyo, Mhe. Jocktan Cheligah, alitumia fursa hiyo kumshukuru Mhe. Simbachawene kwa utayari wake wa kukubali kusaidia kutatua changamoto zinazoikabili shule hiyo ambayo imekuwa mkombozi kwa Wananchi anaowaongoza.



*Baadhi ya muonekano wa majengo ya shule ya Sekondari Lumuma Green ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi wa Kata ya Lumuma katika Jimbo la Kibakwe mkoani Dodoma ambapo amewapongeza wananchi hao kwa kazi kubwa waliyofanya.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mbunge wa Kibakwe ambaye pia Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, Mhe. George Simbachawene akisalimiana na wananchi wakati wa mkutano wa hadhara katika Kata ya Lumuma.*



*Sehemu ya wananchi wa Kata ya Lumuma wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mbunge wa Kibakwe ambaye pia Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, Mhe. George Simbachawene wakati wa mkutano wa hadhara katika Jimbo la Kibakwe.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, Mhe. George Simbachawene akimtambulisha mke wake wakati mkutano wa hadhara katika Kata ya Lumuma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, Mhe. George Simbachawene akizungumza na Walimu wa Shule ya Sekondari Lumuma Green ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi wa Kata ya Lumuma katika Jimbo la Kibakwe mkoani Dodoma kabla ya mkutano wa hadhara.*



*Baadhi ya Madiwani wa viti Maalum wa CCM wa Kata ya Kibakwe wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mbunge wa Kibakwe ambaye pia Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, Mhe. George Simbachawene wakati wa mkutano wa hadhara katika Jimbo la Kibakwe.*

# WAZIRI MKENDA AFANYA ZIARA SEKONDARI YA WAMA SHARAF

**Na. Mwandishi Wetu – Lindi.**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amefanya ziara katika Shule ya Sekondari ya WAMA Sharaf iliyopo mkoani Lindi kujionea hali ya utoaji elimu shuleni hapo.

Akiwa shuleni hapo Waziri Mkenda aliwaasa Wanafunzi kusoma kwa bidii na kuwa na maadili kwani ndio msingi wa mafanikio.

"Mafanikio yanaanza na nidhamu, niwaombe tudumishe nidhamu, tusome kwa bidii ili kufikia malengo mliyojiwekea." Alisema Prof. Mkenda.

Waziri Mkenda aliipongeza Taasisi ya WAMA kwa kuwezesha Watoto wa Kitanzania ambao pengine wasingeweza kusoma kutokana na changamoto za kimazingira kupata elimu na kwamba Serikali itashirikiana nao kuhakikisha watoto hao wanapata elimu bora.









# WAZIRI MKENDA ASEMA ELIMU NI MTAJI KWA TAIFA KUSONGA MBELE

**Na. Mwandishi Wetu – Tanga.**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema elimu ndio mtaji na kwamba ndiyo itawezesha na kubadilisha Taifa liweze kusonga mbele.

Waziri Mkenda alisema hayo Mkoani Tanga alipokuwa akizindua Kampeni ya 'Niache Nisome Pangani Inanitegemea' iliyobuniwa na Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Mhe. Zainabu Abdallah.

Alisema nchi inahitaji Wataalam wazuri katika fani mbalimbali akitolea mfano Madaktari, Walimu na Wahandisi ili iweze kusonga mbele hivyo ni vizuri kuwaacha watoto wasome ili waweze kutimiza ndoto zao.

"Elimu ni ufunguo wa maisha ukimnyima mtoto elimu unamnyima maisha kwani mafanikio ya watu waliosoma ni chachu katika kuleta mabadiliko." Alisema Prof. Mkenda.

Akizungumzia Kampeni ya 'Niache Nisome Pangani Inanitegemea' inayofanyika katika Halmashauri ya Pangani Mkoani Tanga, Waziri Mkenda alimpongeza Mkuu wa Wilaya hiyo Mhe. Zainabu Abdallah pamoja na Mbunge wa Jimbo hilo Jumaa Aweso na kusema kuwa kuna la kujifunza kutoka katika halmashauri hiyo ili kuleta mageuzi ya elimu na amehimiza watu kujifunza kwenye mambo mazuri kama hayo.

Kufuatia ombi la Mhe. Aweso kuhusu VETA ya Wilaya hiyo kuanza kutoa mafunzo Prof. Mkenda amemuahidi kuhakikisha VETA zote za Wilaya za Mkoa wa Tanga zinaanza kutoa mafunzo mwezi Septemba mwaka huu 2023.




Pia alisema kuwa kwa maelekezo ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu kuweka Kampasi za Vyuo Vikuu katika Mikoa 14 ambayo haina na vyuo hivyo, Tanga inakwenda kupata Kampasi ya Chuo Kikuu Mzumbe.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Mhe. Husna Sekiboko, alimuomba Waziri Mkenda kuupa Mkoa wa Tanga kipaumbele kwa fursa za elimu hasa Wilaya ya Pangani kwa kuwa ni moja ya wilaya ambayo wanafunzi wanatembea umbali mrefu kufuata shule.

"Mhe. Waziri wanafunzi wanatembea umbali mrefu kuifuata shule katika wilaya hii. Niliamua kutoa fedha zangu kuwaweka hostel kutokana na changamoto hiyo ili kuwaepusha na vishawishi njiani. Naomba fursa yoyote ikitokea ilete Pangani." Alisema Mhe. Sekiboko.

Nae Mbunge wa Jimbo hilo Mhe. Jumaa Aweso, alimshukuru Waziri Mkenda kwa kuwajengea VETA ya Wilaya na kumuomba amfikishie salamu hizo kwa Mhe. Rais huku akimuomba kuifanya Shule ya Funguni iliyopo Wilayani humo kuwa na Kidato cha Tano na Sita.

Nae Mkuu wa Wilaya hiyo Zainabu Abdallah, alisema katika Halmashauri hiyo wameamua kuifanya elimu kuwa kipaumbele kutokana na wilaya hiyo kuwa nyuma kielimu na kwamba kupitia Kampeni waliyoianzisha ya 'Niache Nisome Pangani Inanitegemea' Halmashauri hiyo itakuwa na mageuzi makubwa kwenye elimu.




HASSAN


HERI
foundation

# DKT. MSONDE AINYOOSHEA KIDOLE WILAYA YA KILOMBERO KWA UCHELEWESHAJI WA MIRADI YA ELIMU

- Halmashauri za Mji wa Ifakara na Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba Wilayani Kilombero kikaangoni ujenzi wa miundombinu;
- Amuagiza Mkuu wa Wilaya ya Kilombero kusimamia maeneo yote ujenzi ufanyike usiku na mchana;
- Upanuzi wa Shule za Sekondari kwa Wanafunzi wa Kidato cha Tano ulipaswa kukamilika Julai 30, 2023;
- Wanafunzi wa Kidato cha Tano walipaswa kuanza masomo Agosti 13, 2023.

**Na. Mwandishi Wetu – Kilombero.**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Elimu), Dkt. Charles Msonde amezinyooshea kidole Halmashauri za Mji wa Ifakara na Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba Wilayani Kilombero kwa ucheleweshaji wa ujenzi wa miundombinu ya elimu ya msingi na Sekondari.

Dkt. Msonde alionyesha hali ya kutoridhishwa na kasi ya utekelezaji wa miradi ya elimu ambayo inaendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Kilombero Mkoani Morogoro hivi karibuni katika ziara yake ya kikazi.

"Halmashauri ya Mji wa Ifakara na Mlimba bado mpo nyuma sana katika utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya elimu msingi kupitia mradi wa BOOST na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya Wanafunzi wa Kidato cha Tano." Alisema Dkt. Msonde.

Dkt. Msonde alisema maeneo mengine ya nchi yanayotekeleza miradi hiyo yameshakamilisha na wengine waliochelewa wapo katika hatua za kumalizia kwa kupaka rangi lakini katika halmashauri hizo bado wapo nyuma sana.



Aidha, alisema katika ujenzi wa miundombinu ya Upanuzi wa Shule za Sekondari kwa ajili Wanafunzi wa Kidato cha Tano bado wako nyuma ambapo miundombinu yote inapaswa kukamilika ifikapo Julai 30, 2023 ili iweze kupokea wanafunzi hao watakaoanza masomo Agosti 13, 2023.

Kutokana na hali hiyo, Dkt. Msonde amemuagiza Mkuu wa Wilaya ya Kilombero kuhakikisha anasimamia maeneo yote ambayo bado yapo nyuma katika ujenzi ikiwa ni pamoja na kufunga taa zenye mwanga ili kazi ya unjenzi ifanyike usiku na mchana bila kuathiri ubora na viwango vinavyotakiwa.

Kadhalika, ameagiza maeneo yote ya ujenzi kuongezwa nguvu kazi ya mafundi ili kufanya kazi kubwa zaidi kwa muda mfupi ikiwa ni pamoja na kufanya kazi zinazoenda sambamba kwa wakati mmoja.

Dkt. Msonde amewataka Wakurugenzi na Wahandisi wa Halmashauri hizo kwa kushirikiana na Maafisa Elimu kuweka uangalizi wa karibu kwa kusimamia na kukagua kila hatua inayoendelea katika ujenzi wa miundombinu hiyo.




**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania